



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI**



**S.L.P 42  
SINGIDA**

**Kumb. Na-.IDC/A.1/71/08**

**Tarehe: 29/05/2024**

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Kufuatia Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kupata kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA. 228/613/01/B/056 cha tarehe 15 Machi, 2024 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Ikungi anatangaza nafasi ya kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye Sifa za kujaza nafasi kama ilivyoorodheshwa kwenye Tangazo hili.

**1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - (NAFASI 1)**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada/Cheti (Technician Certificate NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora wa Kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali

- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji, na
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

### 1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA:

Mshahara wa kuanzia ni kima cha serikali katika ngazi ya **TGS. B1**

### 2.0 MASHARTI YA JUMLA:

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiopungua Miaka Kumi na Nane (18) na usiozidi miaka Arobaini na Tano (45).  
**Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**
- ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (**Referees**) watatu wa kuaminika
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni kidato cha Nne, kidato cha Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.  
**Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate, - vyeti vya kitaaluma (professional Certificate from respective boards)**
- v. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU/NACTE na NECTA**
- vi. "Testimonials", Provisional Results, Statement of Results, Hati za matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) HAVITAKUBALIWA.
- vii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na.CAC45//257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010

- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa umma hawaruhusiwi kuomba isipokua kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria
- x. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 11 June 2024.
- xi. **MUHIMU** kumbuka kuambatanisha Barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, Anuani ya Barua hiyo ielekezwe kwa;

MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI,  
S.L.P 42,  
SINGIDA.

xii. *Maombi yote yatumwe kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia Anuani ifuatayo <http://portal.ajira.go.tz>, Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa “Recruitment Portal”.*

xiii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioidhinishwa katika Tangazo hili Hayatafanyiwa Kazi**

xiv. Limetolewa na;

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI**

---

Baruapepe: [ded.ikungidc@singida.co.tz](mailto:ded.ikungidc@singida.co.tz) Website: [www.ikungidc.go.tz](http://www.ikungidc.go.tz)  
Nukushi: 06262964036, Simu:+255262964037/255262964036